

## **Fundisho la Kristo**

### **Uhusiano kati ya Mungu na Mwanawe mkubwa**

Sababu yetu kuwaweka maandiko na nuku hizi katika hili somo si ya kuwa tofauti, wala kuwa na ugomvi. Sababu ni kuwasaidia kuelewa vizuri uhusiano aliokuwa nao Yesu Kristo Mwana wa Mungu na Babake, alivyojitoa kabisa “katika kunena kwake”, “katika vitendo vyake”, “katika fundisho lake” na “katika mapenzi yake” kwelekeaa kunena, vitendo, fundisho na mapenzi ya babake.

Ndugu Branham alitufundisha ya kwamba **Yesu Kristo ndiye kielezo chetu**, lakini tukitazama tu sehemu ya uungu iliyokaa ndani yake, kamwe hatutaelewa tunavyoweza kuwa kielezo kwa jinsi hiyo. Tunapomuona Mwana wa Mungu kama mwana mtiifu, twaweza kuona kile kielezo kinachowapasa wana wote kusawazishwa nacho. Hili ndilo kusudi la kuelewa Uungu. Si kwa minajili ya elimu ya dini, bali kwa ajili ya kuelewa uhusiano wetu na Baba yetu kama Yesu alivyoonyesha jinsi ya kuwa wana watifu. Unaposoma ukiftia somo hili, tafadhalii kuwa mwangalifu kila mara kuona kielezo cha wana wote katika Yesu Kristo. Mungu akubariki katika kusoma kwako.

**2 Yohana 8-9:** *8 Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyoyatenda, bali mpokee thawabu timilifu. 9 Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya* (fundisho la) **Kristo**, *yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho* (fundisho hilo) **hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.** *10 Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho* (fundisho hilo) **hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu.**

Haya ni maneno mazito kutoka kwa mtume Yohana, bali yaliyo muhimu sana kwa mmoja kufungua nayo masikio ya kusikia. Kwa sababu alisema kama hauna lile **Fundisho la Kristo**, basi hauna wala haufuatishi sauti ya maneno ya Mungu. Halafu alisema lile **Fundisho la Kristo** ni Mungu mmoja aliyekuwa na mwana. Alisema kwamba ili kuwa na lile **Fundisho La Kristo**, ni lazima uwe na yule Baba na yule Mwana **pia**. Neno **Pia** linamaanisha ni wawili, mmoja ambaye ni Mungu, na mwingine ambaye ni mwana wa Mungu aliye mzaliwa wa kwanza wa kiume.

**No.1) Kuna Mungu mmoja tu naye ndiye Yule Baba wa Yesu Kristo.** Utu wa mmoja tu aliye Mungu, kuna mungu mmoja tu.

**Kutoka 20:2-3 Mimi ni Mungu wako, Usiwe na miungu mingine.**

**Kumbukumbu La Torati 6:4 Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.**

**Yohana 17:3 Mungu wa pekee wa kweli, Yohana 8:54 ni Mungu wenu**

**Isaiah 54:5 na Mtakatifu wa Israeli, si wawili, si watatu bali mmoja**

**Warumi 15:6 Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.**

**Waebrania 1:9 Mungu, Mungu wako, Zaburi 50:7 Mimi ndimi niliye MUNGU, Mungu wako.**

**Yohana 20:17 Mungu wangu naye ni Mungu wenu**

**1 Wakorintho 8:6 Mungu ni mmoja tu, aliye Baba,**

**1 Wakorintho 1:4 neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu; & 24 Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu.**

**2 Wakorintho 1:3 Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,**

**Waefeso 1:17 Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo,**

**Waefeso 4:6** *Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote,*  
**1 Wathesalonike 3:13** *Mungu, Baba yetu,*  
**2 Wathesalonike 2:16** *Mungu Baba yetu,*  
**Yakobo 3:9** *Mungu Baba yetu,*  
**1 Yohana 3** *zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Yesu Kristo Mwana wa Baba,*  
**Ufunua 3:12** *hekalu la Mungu wangu, jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu,*

**No.2) Yesu ana Mungu.** Mungu ni mwenye enzi, haajibiki kwa yejote. Hana mwingine juu yake aliye Mungu. Kwa hivyo, kama Yesu (Yule mwana wa Mungu) ni Mungu, basi kwa nini yeye hunena kuhusu mwingine aliye Mungu? Na ikiwa Yesu ana Mungu, basi huyu Mungu ni nani kama Yesu mwenyewe ni Mungu? Kwa hivyo, Yesu hakuwa “Mungu Mwana”, bali alikuwa “Mwana wa Mungu” Alikuwa na Mungu na huyo Mungu alikuwa Babake na huyo Babake alikaa ndani yake.

**Yohana 20:17** *Mungu wangu naye ni Mungu wenu*  
**Ufunuo 3:12** *hekalu la Mungu wangu, jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu,*  
**Zaburi 22:1** *Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha?*  
**Marko 15:34** *Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*  
**Matayo 27:46** *Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?*

“*ku-achana*” maana yake ni “*kutupa kabisa*”. Mungu aweza kujitupa mwenyewe?

**1 Wakorintho 11:31** *Mungu, Baba wa Bwana Yesu,*  
**Waefeso 1:3** *Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**Waefeso 1:17** *Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**1 Petro 1:3** *Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**Waebrania 1:8, 9** *Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta,*  
**Zaburi 45:6, 7** *MUNGU, Mungu wako, amekupaka mafuta,*  
**Ufunuo 1:6** *kwa Mungu, naye ni Baba yake;*  
**2 Wakorintho 1:3** *Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**Waebrania 5:7, 8** *alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti,*  
**Luka 6:12** *usiku kucha katika kumwomba Mungu.*  
**Matayo 11:25** *Baba, Bwana wa mbingu na nchi,*  
**Yohana 17:1** *Baba, saa imekwisha kufika.*  
**Matayo 26:39, 42** *Baba yangu, ikiwezekana,*

**No. 3) Yesu kamwe hakudai kuwa Mungu, Yesu alidai kuwa “Yule Mwana wa Mungu”.**

**Zaburi 45:6-7** *Mungu, Mungu wako, amekupaka mafuta,*  
**Mathayo 16:16** *Mwana wa Mungu aliye hai.*  
**Yohana 8:54** *Baba yangu, ambaye ninyi mwanena kuwa ni Mungu wenu.*  
**Yohana 10:36** *Mimi ni Mwana wa Mungu?*  
**Waefeso 1:3, 17** *Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**Waebrania 1:8** *kwa habari za Mwana asema,*  
**Waebrania 1:9** *Mungu, Mungu wako,*  
**Warumi 15:6** *Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.*  
**1 Wakorintho 8:6** *lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba,*

**2 Wakorintho 1:3, 11:31** *Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**2 Wakorintho 1:3** *Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**1 Petro 1:3** *Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,*  
**Petro 1:17** *kwa Mungu Baba heshima na utukufu ... Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA wangu,*  
**2 Yohana 1:3** *Mungu Baba na kwa Yesu Kristo Mwana wa Baba,*  
**2 Yohana 1:9** *huyo ana Baba na Mwana pia.*  
**Ufunuo 1:6** *kwa Mungu, naye ni Baba yake;*

Na vipi kuhusu Yesu mwenyewe, alikuwa na yapi ya kusema kuhusu uhusiano wake na babake?

**Yohana 20:17** *Baba yangu naye ni Baba yenu; kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu*  
**Yohana 2:16, , 5:17,43, 6:32,65, 8:19,28,38,49,54, 10:17,18,25,29,30,32,37,**  
**12:26,14:2,7,12,20,21,23, 15:1,8,10,24, 18:11,20:21** “*Baba yangu*”

**No.4) Yesu alikuaje mmoja na Mungu? Jibu:** Mungu ni Neno, na neno la Mungu ni Uhai, **Na** Yesu hudhihirisha Neno la Mungu na Uhai wa Mungu. Ule Uhai unaotokana na Mungu.  
**Yohana 10: 30-38** *mimi na Baba tu umoja, Baba yu ndani yangu...*  
**Yohana 14:8-10** *aliyeniona mimi amemuona Baba, Baba yu ndani yangu,*  
**Mathayo 12:18** *Moyo wangu uliyependezwa naye, nitatia roho yangu juu yake,*  
**Marko 1:11** *Wewe ndiwe Mwanangu, mpPENDWA wangu, nimependezwa nawe...*  
**Mathayo 17:5** *Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA wangu, ninayependezwa naye...*  
**Mathayo 3:17** *Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA wangu, ninayependezwa naye...*  
**Yohana 17:11** *ili wawe na umoja kama sisi tulivyo. Yohana 17:21* *Wote wawe na umoja; kama wewe, baba ulivyo ndani yangu, name ndani yako; hao nao wawe ndani yetu: 22 Nami Utukufu ule ulionipa **nimewapa wao**; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja:* Tu umoja na Mungu kwa kupokea utukufu wake. *Utukufu* = Kiyunani “*doxa*” inayomaanisha shauri, dhani bora, hukumu za Mungu.

**No. 5) Mungu ni mkuu kuliko Yesu.** Yesu alikuwa chini ya Baba.

**Yohana 10:29** *Baba yangu ni mku Kuliko wote*  
**Yohana 14:28** *kwa maana Baba ni mkuu kulko mimi*  
**Mathayo 20:23** *waliowekewa tayari na Baba yangu*  
**1 Wakorintho 15: 24-28** *chini ya Baba*  
**Zechariah 3:8** *mtumishi wangu aitwaye chipukizi*  
**Mathayo 12:18** *tazama mtumishi wangu niliyemteuwa*  
**Wafilipi 2:7, 8** *namna ya mtumwa*  
**Warumi 5:19** *kwa kutii kwake mmoja*  
**Waebriania 1:9** *Mungu wako amekutia mafuta*  
**Zaburi 45:6-7** *Mungu wako amekupaka mafuta*  
**Luka 6:12** *usiku kucha katika kumwomba Mungu*  
**Mathayo 11:25** *Baba, Bwana wa mbingu na nchi*  
**Yohana 17:1** *Baba, sasa imekwisha kufika*  
**Mathayo 26:39, 42** *Baba yangu, ikewezezana*  
**1 Wakorintho 11:3** *kichwa cha Kristo ni Mungu*  
**1 Wakorintho 3:23** *na Kristo ni wa Mungu*  
**Mathayo 20:23** *sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu*

## **1 Wakorintho 15:24-28 mwana mwenyewe yu chini ya Baba**

Yesu anakiri ya kwamba Baba yake ni mkuu kuliko yeye. Neno hili Mkuu limetafsiriwa kutoka kwa neno la kiyunani ambalo halimaanishi tu “**mkuu**” bali pia “**mkubwa kwa umri**”.

Mwaminio wa fundisho la utatu anapokwambia ya kwamba Yesu aliishi milele na kwamba alikuwa sawa na babake, awezaje ikiwa mwana mwenyewe alikanusha. Wana wote wana mwanzo. Basi Mwana angewezaje kuwa Baba wa Milele?

**Isaiah 9:6 (A)** “*Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa*”, kama amezaliwa, basi ana mwanzo, kwa hivyo si wa milele...kama amezaliwa kuna mwingine kabla yake wa kumzaa. Kuzaliwa kunaleta fikira za kuhesabiwa kwa jamii na ukoo, pia inaashiria kuzaa.

**(B) Tumepewa (mtoto) mwanaume.** Yeye ni kipawa, mwenye kupeana ni mkuu kuliko kipawa.  
Yohana 3:16

**(C) Uweza wa kifalme utakuwa (au serikali itakuwa) begani mwake Luke 1:32 ataitwa mwana wa aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, babake.**

**(D) Naye ataitwa jina lake Mshauri, wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.** Hebu sasa tuhoji sehemu ya mwisho inayohusika na jina la huyu mtoto. Mtoto huyu mwanaume atakaezaliwa: **Wa ajabu** (wa ajabu ni jina? La hasha) **Mshauri** (Mshauri ni jina? La hasha. Ni cheo.) **Mungu mkuu**, (Mungu mkuu ni jina?) **Baba wa milele**, (Baba wa milele ni jina, La hasha!) **Mfame wa Amani** (Mfalme wa Amani ni jina? La hasha) Sasa, kuna jina moja la Baba wa Milele, Mungu mkuu, Mshauri, na kadhalika. Jina hilo ni Yesu. Basi sasa “**ataitwa**” jina lake ni kumaanishaje? Neno “**ataitwa**” lilitafsiriwa kutoka kwa neno la Kiebrania “**qara**” linalomaanisha “**kutangaza**” *Jina lake litatangaza Yule Mungu mkuu, Baba wa milele. Jina la Babake.*

**No.6) Yesu alikuja kwa jina la Babake.** Jina la Babake ni Yesu.

**Yohana 5:43, 10:25 Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu,**

Kwa hivyo jina la Baba lilikuwa Yesu, jina lile lile alilopewa Mwana. Mtume Paulo alisema “*Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake*” Hakusema **Mungu alikuwa Kristo bali** “*Mungu alikuwa NDANI YA Kristo*”

**1 Wakorintho 5:19** “*Mungu alikuwa ndani ya Kristo*” Anayofundisha Paulo hapa si kwamba Yesu alikuwa utimilifu wa Uungu, bali anafundisha ya kwamba **NDANI** yake kulikaa utimilifu wa Uungu.

**Wakolosai 2: 9 Ndani yake unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.** Petro hakufundisha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa Yesu, bali alishuhudia Mungu Baba alinena na kusema kwamba Alishuka chini na akakaa **ndani** ya mwanawе.

**2 Petro 1:17 alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, Huyu ni Mwanangu,**  
**Yohana 10:25 Kazi hizi ninazozifanya kwa jina la Baba yangu ndizo zinazonishuhudia.**

**No.7) Yesu aliomba kwa Babake aliye Mungu.**

**Yohana 14:16, Yohana 16:26, Yohana 17:9, 15, 20, ninaowaombea Mathayo 6:9, Mathayo 11:25, Mathayo 14:23, Mathayo 26:36, 39, 42, 53, Luka 6:12, Luka 9:28, Luka 11:2 Marko 6:46, Waerbrania 5:7, 8**

**No.8) Mwana wa Mungu angejifunza, angejiongezea maarifa**

**Waebrania 5:8 na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii**

**Luka 2: 52 Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo,**

**No.9) Yesu alitii Baba yake kwa mambo yote.** Mungu hawezi kumtii yejote zaidi yake mwenyewe kama yeye ni Mungu aliye pekee Mwenye enzi zote.

**Waebrania 5:8 na, ingawa ni Mwana, alijifunza kutii**

**Yohana 5:17 Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi.**

**Yohana 5:19 Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda;**

**Yohana 5:30 Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe;**

**Yohana 8:29 nafanya sikuzote yale yampendezayo.**

**Yohana 10:18 Agizo hilo nalilipokea kwa Baba yangu.**

**Yohana 10:32 kazi njema nyangi nimewaonyesha, zitokazo kwa Baba;**

**Yohana 12:49 Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema.**

**Yohana 12:50 kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo.**

**Yohana 14:31 na kama vile Baba alivyonihamuru;**

**No.10) Yesu alifanywa mkamilifu.** Hii ni kumaanisha mwana wa Mungu aliweza kubadilika katika kimo, hekima na ukomavu.

**Waebrania 5:9 naye alipokwisha kukamilishwa, kama alikamilishwa basi hakuzaliwa vile.**

**Malaki 3:6 na Waebrania 13:8 Mungu hawezi kubadilika. Luka 2:40 Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Luka 2:52 Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, (ubivu) akimpendeza (shawizi) Mungu na wanadamu.**

**No.11) Yesu hakuwa Ajuaye yote, Mungu ndiye Ajuaye yote.**

**Isaya 40:13, 14 Yesu alipokea maarifa kutoka kwa Mungu**

**Yohana 8:28 ila kama Baba alivyofundisha ndivyo ninenavyo.**

**Marko 13:32 habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye...ila Baba.**

**Mathayo 24:36 habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye...ila Baba.**

**Luka 2:52 Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo,**

**Yohana 5:19 Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda;**

**No.12) Mwana wa Mungu ametiishwa chini ya Mungu kwa mambo yote.**

**1 Wakorintho 15:28 naye Mwana atakuwa chini ya Mungu ambaye ameviweka vitu vyote chini yake, ili Mungu awe yote katika yote.**

**Yohana 5:19 Mwana hawezi kufanya jambo lo lote mwenyewe**

**Yohana 5:30 Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe**

**Yohana 8:29 nafanya sikuzote yale yampendezayo.**

**Yohana 10: 18 ni amri niliyopokea kutoka kwa Baba yangu.**

**Yohana 12:49 Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema.**

**Yohana 12:50 kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo.**

**Yohana 14:31 na kama vile Baba alivyonihamuru;**

**No.13) Yesu alimtegemea Baba kuregesha Utukufu wake.**

**Yohana 17:5** *Na sasa, Baba, unitukuze mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako.* Hiyo ni kesema kwamba alikua nao lakini alisimama kando nao uondoke, na sasa anauliza aregeshewe tena. Jambo la muhimu kutambua ni kwamba alijivua haki zote alipokuja ardhini kuchukua namna ya mwanadamu, akajimimina kabisa na kuchukua maumbile ya mtumwa. Ile tafsiri ya Weymouth inasema “*ingawa kutoka mwanzoni alikuwa na maumbile ya Mungu, hakuhesabu usawa na Mungu kuwa kitu cha thamani kifaacho kufumbatiwa, ila alijivua Utukufu wake, akajichukulia maumbile ya mtumwa aliye kifungoni, mwanadamu kama wanadamu wengine.*” Akiwa mtumwa kifungoni, sifa kuu iliyojieleza ni kujitoa kwa ajili ya mapenzi ya aliyemweka kifungoni.

**No.14) Yesu alitegemea mapenzi ya Mungu Baba yake.**

**Waembrania 10:7** *nimekuja Niyafanye mapenzi yako, Mungu.*

**Waembrania 10:9** *nimekuja niyafanye mapenzi yako.*

**Luka 11:2** *Mapenzi yako yatimizwe,*

**Luka 22:42** *walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke.*

**Mathayo 6:10** *Mapenzi yako yatimizwe,*

**Mathayo 26:42** *mapenzi yako yatimizwe.*

**Mathayo 7:21** *bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*

**Mathayo 12:50** *ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu*

**Yohana 5:30** *bali mapenzi yake aliyenipeleka.*

**Yohana 6:38** *bali mapenzi yake aliyenipeleka.*

**Yohana 8:29** *kwa sababu nafanya sikuzote yale yampendezayo.*

**No. 15) Mungu na Yesu si mmoja vile kidole chako kilivyo kimoja**

**Yohana 5:31, 32** *wawili wanatoa ushuda; Yuko mwingine anayenishuhudia;*

**Yohana 5:36** *Lakini ushuhuda nilio nao, zanishuhudia ya kwamba Baba amenituma.*

**Yohana 5:37** *Naye Baba aliyenipeleka amenishuhudia.*

**Yohana 8:16** *bali ni mimi na yeye aliyenipeleka.*

**Yohana 8:17-18** *Ushuhuda wa watu wawili ni kweli. Mimi ndimi ninayejishuhudia mwenyewe, naye Baba aliyenipeleka ananishuhudia.*

**No.16) Yesu alimtegemea Baba yake kwa mafunzo yake.**

**Yohana 7:16** *Mafunzo yangu si yangu mimi,*

**Yohana 10:18** *ila ni yake yeye aliyenipeleka.*

**Yohana 12 :49** *Agizo hilo nalilipokea kwa Baba yangu.*

**Yohana 12:50** *Baba ameniagiza nitakayonena na nitakayosema.*

**Yohana 14:31** *kama vile Baba alivyoniamuru; ndivyo nifanyavyo*

**No.17) Baba alimtuma Mwana.**

**1 Yohana 4:1** *Baba alimmtuma Mwana kuwa mwokozi wa ulimwengu*

**Yohana 5:23, 5:30, 5:36, 5:37** *Baba amenituma. Baba aliyenipeleka*

**Yohana 6:39, 6:44, 6:57** *Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi,*

**Yohana 20:21** *kama Baba alivyonituma mimi,*

**Yohana 8:16, 18** *Baba aliyenipeleka.*

**Yohana 8: 29, 42** *yeye ndiye aliyenituma.*

**Yohana 10:36** *Yeye ambaye Baba alimtakasa, akamtuma ulimwenguni,*

**Yohana 12:49** Baba aliyenipeleka,  
**Yohana 14:24** Baba aliyenipeleka.  
**Yohana 17:21, 17:25** upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.

**No. 18) Mungu alimfufua Yesu katika wafu, hakujifufua mwenyewe**  
**Matendo ya Mitume 2:24** ambaye Mungu alimfufua  
**Matendo ya Mitume 3:15, 26** Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu,  
**Matendo ya Mitume 5:30** Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu,  
**Matendo ya Mitume 10:40** Huyo Mungu alimfufua siku ya tatu,  
**Matendo ya Mitume 13:23, 13:30, 13:34, 13:37** Mungu alimfufua  
**Matendo ya Mitume 17:31** kwa kumfufua katika wafu.  
**Waefeso 1:20, 2:6** alipomfufua Yesu  
**Warumi 4:24, 6:4, 8:11, 10:9** Mungu alimfufua katika wafu  
**Wagalatia 1:1** Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu  
**1 Wakorintho 6:14** Naye Mungu alimfufua, **15:15** Mungu ya kuwa alimfufua Kristo  
**2 Wakorintho 4:14** ye ye ali yemfufua Bwana Yesu  
**Wakolosai 2:12** Mungu ali yemfufua katika wafu  
**1 Petro 1:21** Mungu, ali yemfufua katika wafu  
**1 Wathesalonike 1:10** alimfufua katika wafu

**No.19) Yesu alikufa, Mungu hawezi kufa**  
**2 Wakorintho 4:10** kuuawa kwake Yesu,  
**1 Wathesalonike 4:14** Yesu alikufa akafufuka,  
**Yohana 19:40** Walizika mwili wa Yesu  
**Yohana 12:7, Marko 9:31, Marko 10:34** Yesu alinena kuhusu kifo chake  
**Yohana 19:34** walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa,  
**1 Wakorintho 15:3** **1** Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, **Timotheo 6:15-16** ambaye ye ye peke yake hapatikani na mauti, **1 Timotheo 1; 17** kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyekana, Mungu peke yake

**No. 20) Yesu aliona njaa, aliona kiu alichoka, Mungu ni Roho**  
**Mathayo 4:10** Yesu akaona njaa  
**Marko 11:12** aliona njaa.  
**Yohana 19:28** aliona kiu  
**Yohana 4:6** amechoka kwa safari yake,  
**Zaburi 121:3, Zaburi 121:4** Mungu hawezi Kulala usingizi, wala kusinzia

**No. 21) Yesu alijaribiwa, Mungu hawezi kujaribiwa**  
**Mathayo 4:1** Yesu alijaribiwa  
**Marko 1; 13** Yesu alijaribiwa  
**Luka 4:2** muda wa siku arobaini nyikani, akijaribiwa na Ibilisi

**No. 22) Yesu alipata mateso, Mungu hawezi kuteswa**  
**Luka 24:26, 24:46** Haikumpasa Kristo kupata mateso  
**Matendo ya Mitume 3:18, 17:3, 26:23** Kristo hana budi kuteswa  
**1 Petro 1:11** mateso yatakayompata Kristo

**1 Petro 3:18** *Kristo naye aliteswa mara moja*

**1 Petro 4:1, 4:13** *Kristo aliteswa*

**1 Petro 5:1** *mateso ya Kristo,*

**No. 23) Mwana alipokea uhai kutoka kwa Baba** Baba ni mwanzilishi wa uhai

**Luka 1:35** *hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu.*

**Yohana 5:26** *vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake.*

**Yohana 6:57** *Kama vile Baba aliye hai alivyonitura mimi, nami ni hai kwa Baba;*

**No. 24) Mwanadamu Yesu ni mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu**

**1 Timotheo 2:5** *mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Yesu*

**Wagalatia 3:20** *aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja; bali Mungu ni mmoja. Wa tatu katika ugonvi wa wengine*

**No. 25 Mungu alimwinua Yesu** ye yote atakayejikweza, atadhiliwa

**Wafilipi 2:9** *Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno*

**Matendo ya Mitume 2:33, 5:31** *huyo Mungu amemtukiza*

**Mathayo 23:12, Luka 14:11, 18:14** *ye yote atakayejikweza, atadhiliwa*

**No. 26) Yesu ametiwa mafuta na Mungu Babake awe Bwana na Kristo pia**

**Luka 1:31-33** *Mungu atampa kiti cha enzi*

**Yohana 5:22, 5:27** *Baba amempa Mwana hukumu yote*

**Matendo ya Mitume 2:36** *Mungu amemfanya Yesu huyo kuwa Bwana na Kristo.*

**Matendo ya Mitume 10:38, 10; 42** *Mungu alimtia mafuta Yesu kwa Roho Mtakatifu*

**Matendo ya Mitume 17:31** *Mungu atahukumu kwa mitu yule aliyemchagua;*

**No. 27) Mwana wa Mungu si mwenye enzi, Mungu ndiye mwenye enzi**

**Yohana 5:17** *Yesu alilaumiwa na wayahudi kwa kufanya kazisiku ya sabato kwa sababu aliponya siku ya sabato. Jibu lake lapatikana katika aya ya 17 Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi. 18 Basi kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu. Basi Yesu akajibu, akawaambia, Amin, amin, nawaambia, 19 Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.* Yesu anaambia wayahudi kwamba yeye hana uwezo mpaka Baba amuonyeshe la kufanya. Anasema, Mwana hawezi kutenda **lolote**. Basi mwana hawezi kuokoa, hawezi kuponya, hawezi kukombowa, hawezi kufanya lolote, mpaka aonyeshwe na Baba la kufanya. Haya si maneno ya aliye mwenye enzi.

Lakini mungu ni Mwenze enzi, anayejua yote na aliye na uwezo wote.

1. Mwenye enzi haitikii yeyote.
2. Mwenye enzi hutawala na mamlaka kuu juu ya yote
3. Mwenye enzi ana uhuru wa kujitawala kando na wengine wote

Kwa hivyo, Mwana wa Mungu si mwenye enzi, Mungu peke ndiye mwenye enzi. Yesu alimtegemea Babake kabisa katika kutenda na kunena. Hakukua na maneno yake, kazi zake, wala mafundisho yake, na alitiisha mapenzi yake mwenyewe kwa Baba. Mungu ndiye Mwenye enzi na alikaa ndani ya mwanawawe aliye mwenyewe kwa mambo yote. Mungu ndiye anayejua yote, Mungu ndiye aliye na uweza wote, lakini mwanawawe mara zote hutegemea Babake kwa kila kitu pamoja na kunena, kutenda, mafundisho yake, na hata kusalinisha mapenzi yake kwa mapenzi ya Babake.

Yesu alisema “*Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke*”, na kadhalika. Hayo si maneno ya aliye mwenye enzi. Maandiko yote yanayonena juu ya mwana huonyesha si Mwenye enzi. **Yohana 5:20** *Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, naye humwonyesha yote ayatendayo mwenyewe; hata na kazi kubwa zaidi kuliko hizo atamwonyesha, ili ninyi mpate kustaajabu.* Tazama Yesu alimtegemea Mungu kumuonyesha ono kuhusu alilopaswa kutenda.

**Yohana 5:21** *Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwahuisha, vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao.* **Yohana 5:21** *Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote.*

**Warumi 15:5** *Na Mungu mwenye saburi na faraja awajalie kunia mamoja ninyi kwa ninyi, kwa mfano wa Kristo Yesu.*

**Yohana 12:44** *Naye Yesu akapaza sauti, akasema, Yeye aniaminiye mimi, haniamini mimi bali yeye aliyenipeleka.*

**Yohana 5:23** *ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba.*  
*Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyenipeleka.* Tunapomheshimu Mwana tunamheshimu Baba, kwa sababu Mwana hutenda tu yale Baba amemwamuru kutenda. Hivyo basi tuonacho ni Baba akifanya kazi na mwana akifanya kazi vile vile. Tunapomheshimu Mwana tunatambua jukumu la Baba lenye sifa ya utangulizi, na jukumu la Mwana la utiifu mkamilfu kwa Baba.

**Yohana 5:24** *Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.*

**Yohana 14:10b** *Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake.*

**Waaminio wa fundisho la utatu** hutumia badhi ya hoja kweleaza jinsi Mungu na Yesu walivyo mmoja kama kidole chako kilivyo kimoja. **Waaminio wa fundisho la umoja** vile vile, lakini kwa mtazamo tofauti. Kwa kuwa **Waaminio wa fundisho la utatu** huona wahusika watatu, wao hujaribu kuwafanya mmoja jinsi ya umbo lenye pembe tatu. Lakini Mungu na Mwanawawe ni mmoja kwa Neno la Mungu.  
Mungu ni Neno, na neno lake lilielezwa kupitia utu wa mwanawawe. Maandiko yafuatayo hutumika na waaminio wa fundisho la utatu kujaribu kueleza utatu Wa Uungu.

**Wafilipi 2:6** ambaye alikuwa yuna namna ya Mungu, **Wakolosai 1:15** naye ni mfano wa Mungu asiyonekana, **2 Wakorintho 4:4** Kristo aliye sura yake Mungu. **Yohana 12:45** Nay anitazamaye mimi amtazama yeye aliyenipeleka. **Yohana 14:9** Aliyeniona mimi amemwona Baba **Wakolosai 1:19** katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae **Wakolosai 2:9** katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, **Waebrania 1:3** chapa ya nafsi yake,

Haya maandiko yanaweza kuvunjwa katika vikundi tofauti vya hoja. Kwanza, wanaamini ya kwamba Yesu alikuwa yuna namna ya Mungu na wanaamini hiyo inamaanisha yeye ni Mungu. Hivyo basi wanatoa sababu, kwa kuwa hawaelewii maneno “namna” na “mfano” kwamba si asili. Hawaelewii uhai wa Mungu.

Biblia inatufundisha Mungu aliweka mwili mzima **Katika** tumbo la uzazi la mwanamke.

**Waebrania 10:5** “*Mwili uliniwekea tayari*” (yaani: yai na mbegu pia) **Waebrania 1:3** mwanadamu Yesu (ule mwili, yule mwana wa Mungu) alizaliwa na kila sifa na tabia iliyokuwa ndani ya Mungu. Kwa maneno mengine, **Mungu alinywesha chembe chembe za nasaba (DNA)** kama twaweza sema hivyo, yote aliokuwa ndani ya kiziwa cha umbile la yule mwana wa Mungu na kwa hivyo ule mwili ulikuwa kwa aina halisi pumzi na uhai wa Baba, lakini hakuwa Baba, bali katika “ule mfano” wa Baba. Na kama ni kwa mfano wake si Baba mwenyewe. Hilo si dokezo hata kidogo ya kwamba Yesu Mwana wa Mungu ni Mungu mwana. “**mfano**” maana yake ni ufanani au **tabia chapa**. Yesu alikuwa dhihirisho la kuonekana kwa uhai wa Mungu ndani ya mwanadamu. Tabia yake ilitoa mangao wa yote aliyo Mungu au kile uhai wa Mungu ungeweza kueleza katika mwili uonekanao. Kwa hivyo, watu wangeweza kujua tabia ya Mungu kwa kuona ikielezwa katika maisha ya Yesu. **I Yohana 1:2** (*na Uzima au uhai huo ulidhahirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwashubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu;*) Uhai wake ulifunua utakatifu, haki, hukumu, upendo, rehema, fadhili, ukweli, unyofu na uaminifu. Yesu alikuwa mtawua; alikuwa kama Mungu katika tabia na mwenendo. Yesu hakuwa Mungu mwenyewe, alitoa mangao wa tabia ya Mungu katika maisha yake.

Yale maandiko yanayosungumzia utimilifu wa Uungu unaokaa ndani ya Kristo hayamfanyi mwanadamu Yesu kuwa Mungu. Mungu ni roho. Yeye si nyama na mifupa. Bali Mungu asiyonekana alikuja chini na kukaa ndani ya Mwanawе Mtoni Jordan mahali Yohana aliona kwa macho ile Nuru, (yaani: *ile Nguzo ya Moto*) alikuja chini na nuru juu ya Yesu ilikaa na kudumu ndani yake. Upako huo ulimuacha katika bustani ya Gethsemane. Ndio maana angelia msalabani kwa Mungu wake, “**Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniachaka.**” Ule upako ulimuondoka ili aweze kufa mauti ya kawaida. Mradi tu Mungu aliishi ndani yake katika ule itimilifu, hangeweza kufa. Walijaribu mara nyangi kumuua bila kufanikiwa.

Katika **Luka 24:39** walidhani Yesu ni Roho, lakini alipowaonyesha mikono yake na miguu, walijua yeye si roho. **Sasa, Mungu ni Roho** lakini Yesu ni mwanadamu ambaye ndani yake yule Roho mkuu mwenye mamlaka alikaa. Baada ya kuwasalimia, Yesu aliwambia, “**kama Baba yangu alivyonitura, mimi nami nawapeleka ninyi.**” Akionyesha ya kwamba yeye si Baba, lakini alitumwa na Baba, na kwa hivyo yu chini ya mamlaka ya Baba. Kwa vile wanaoamini fundisho la utatu hutumia maneno ya Thomaso kuthibitisha ya kwamba Yesu ni Mungu, basi shetani ana haki kutumia maneno ya mafarisayo kwamba Yesu alikufuru, kwa sababu wote

wanapatikana katika maandiko wakinena kuhusu walivyoamini Yesu ndiye. Ushawishi wa aina hiyo hauwezi kusimama dhidhi ya majaribio ya mama ya ushahidi wa maandiko yaliyopeanwa. Ati kwa sababu mtu fulani amesema maneno fulani katika biblia haifanyi hayo maneno kuwa Neno la Mungu. Maandiko yasema Yuda alitoka akaenda kujinyonga, na katika maandiko mengine tunampata Yesu akisema katika **Luka 10:37** “*Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo.*” Kwa hivyo ni lazima tutumie kwa uhalali neno la kweli. Upambanusi haramu wa maandiko huleta kifo cha kiroho.

Andiko lingine ambalo waaminio wa fundisho la utata hutumia ni **Tito 2:13 Tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu.** Walakani andiko hili halineni kuhusu Mwana wa Mungu, bali Yule Baba wa Utukufu kama Paulo anenavyo kuhusu yeze Parousia (kuwapo) katika **Waefeso 1:17 na 1 Wathesalinike 4:15-18.** Kule kuonekana hunena juu ya kuwapo kwa Roho Mtakatifu (**Mungu mwenyewe**) akishuka chini kabla ya kule kuja halisi kwa kimwili kwa Bwana Yesu Kristo. Kunapaswa kuwe na kuonekana kwa yule Baba wa Utukufu hapa chini ardhini kabla hatujaenda kukutana na Mwana wa Mungu hewani (si hapa ardhini) kama ilivyo katika Mwanzo, tuaona kwamba Baba Mungu alionekana kwa nabii wake Ibrahim kabla ya kuja kwa Yule mwana aliyeahidiwa.

Andiko la mwisho linalotumika kila mara na waaminio wa fundisho la utatu ni **KJV Waebrania 1:8 Lakini kwa habari za Mwana asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya usalme wako ni fimbo ya adili.** Sasa, uchunguzi wa makini wa yale mandiko katika kiyunani waonyesha kosa lilitokea katika kutafsiri neno la kiyunani “**PROS**” lililo tafsiriwa kama neno “**kwa**” (*habari za*) ambalo linasungumzia kumwelekeea **yule mwana wa Mungu** badala ya kuwa yalitoka kwake, hivi basi maneno hayo yanaeleweka kuwa yalitoka kwa Mungu kumwelekeea Yule Mwana na si kutoka kwa Mwana wa Mungu kumwendea Babake haswa kama yalivyoandikwa na Mtume Paulo. Neno lililo sawa na lugha sanifu ya kiingereza linalofaa kutumika ni “**Kulingana na**” au “**Kutokana na**”

Basi andiko hilo linapaswa kusomwa hivi, **Waebrania 1:8 Lakini Kulingana na Mwana (au yule Mwana) yeze asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya usalme wako ni fimbo ya adili.** Naye Baba anamjibu **9 Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, (hata) Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio.** Kutiwa mafuta na Mungu juu ya Mwanawe kama ilivyotajwa hapa pia kumethibitishwa katika maandiko mengine mengi. Na mwishowe tunaona mwana anamjibu Baba akisema, **10 Na tena, Wewe, Bwana, hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako:** Kwa hivyo twaweza kuona haya yalikuwa mazungumzo kati ya Mungu na Mwanawe, kama tuonavyo kutoka mwanzo wa sura ya kwanza ya kitabu cha Waebrania.

**Waebrania 1:1 Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, 2 mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka (Mungu alimweka) kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeze (Mungu) aliufanya ulimwengu. 3 Yeye (Yule Mwana wa Mungu) kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake** (Mungu) **na chapa ya nafsi yake** (Mungu), **akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake** (Mungu), **akiisha (Mwana wa Mungu) kufanya utakaso wa dhambi, (yeze, Mwana wa Mungu) aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;** (ambaye ni Mungu) **4 amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi** (Yule Mwana wa Mungu) **lilivyo tukufu kuliko lao.** (kwa hivyo kama alilipata jina lake kupitia urithi,

hakua nalo mwanzoni, bali alipewa jina hilo na Babake) **5 Kwa maana** (Mungu) **alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, Mimi** (Mungu) **nitakuwa kwake** (Yule Mwana wa Mungu) **baba, Na yeye** (yule Mwana wa Mungu) **atakuwa kwangu mwana?** **6 Hata tena,** (Mungu) **amletapo mzaliwa wa kwanza** (yule mwana wa Mungu) **ulimwenguni,** (Mungu) **asema, Na wamsujudu** (Yule Mwana wa Mungu) **malaika wote wa Mungu.** **7 Na kwa habari za malaika** (Mungu) **asema, Afanyaye malaika zake** (Mungu) **kuwa pepo, Na watumishi wake** (Mungu) **kuwa miali ya moto.** **8 Lakini Kulingana na** (yule Mwana wa Mungu) **Mwana asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya usalme wako ni fimbo ya adili.** **9 Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako,** (Mungu wa nani? Mungu wa Mwana wa Mungu) **amekutia mafuta** (Mwana wa Mungu), **Mafuta ya shangwe kupita wenzio.**

Katika tafsiri ya **NIV** tunasoma **Waebrania 1:3** ikitsemwa hivi “**Yule Mwana ni wangavu wa Utukufu wa Mungu, na mfano halisi wa kuaakilisha kuwapo kwake, akiendeleza vitu vyote kwa neno lake la nguvu. Pia tunapata kwa ile tafsiri ya amplified** (ilioboresha) **ya Waebrania 1:3** “**Yeye ndiye peke yale madhahirisho** ya ule utukufu wa Mungu – kiumbe cha nuru - kujitokeza kwa miale ya nuru ya kiungu. **Na yeye ni chapka kamilifu na mfano halisi wa maumbile ya Mungu, akishikilia, na kudumisha na kuongoza na kusukuma dwara kwa neno lake la nguvu za uwezo.**” Tafsiri yejote iliotofauti ingeruka kinyume na ukweli wa maandiko na maneno ya Bwana Yesu Kristo mwenyewe yalionenwa katika **Yohana 17:3** **Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.**

Katika Agano la Kale Mungu anajulikana kama **Mungu Mmoja wa Kweli Yeremiah 10:10** **Bali Bwana ndiye Mungu wa kweli; Ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele:**

Tena anasemekana kuwa **Mungu wa kweli** katika **2 Mambo ya Nyakati 15:3** *Basi tangu siku nyingi Israeli wamekuwa hawana Mungu wa kweli, wala hawana kuhani afundishaye, wala hawana torati.*

**Maandiko wale waaminio wa fundisho umoja** (Yesu peke) wanayotumia kufundisha Yesu **Mwana wa Mungu haswa ndiye yule Baba aliyejigeuza:** **1 Yohana 5:20** “**Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, yaani, ndani ya Mwana wake Yesu Kristo. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele.**”

Sasa, wanaisoma hii kama “**tumo ndani ya Mungu mmoja wa kweli ambaye ni Yesu**” Bali neno “**yaani**” limetumika na kumaanisha “**sawa na vile**” basi msitari huo unapaswa kusemekwa hivi, “**Nasi twajua kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli, sawa na vile** Mwana wake Yesu Kristo alivyo ndani yake. Huyu ndiye Mungu wa kweli, na uzima wa milele.” Hivyo ndivyo Yesu alivyoomba kwa Babake katika **Yohana 17 ili tuwe na umoja kama vile** (sawa na vile) **yeye alivyo kuwa mmoja na Babake.**

**William Branham**, nabii wa Mungu kwa kizazi cha mwisho alijumlisha uhusiano kati ya Mungu Baba mwanawewe Yesu Kristo kwa maneno yafuatayo:

**Ukombozi Mkamilifu 59-0712 Kifungu55** *Kwa ukamilifu Yesu alikuwa, mwanadamu kabisa. Angelia kama mwanadamu, angekula kama mwanadamu; angeweza kufanyika kama mwanadamu. Kwa ukamilifu alikuwa, mwanadamu kabisa katika maumbile yake ya kimwili. Na Katika roho yake, Kwa ukamilifu alikuwa, Mungu kabisa, hivyo basi **akautiisha mwili wake wa nyama kwa roho aliyekuwa ndani yake.** Unaona, alijaribiwa kwa namna zote kama sisi. Alikuwa mwanadamu, si Malailka. Alikuwa mwanadamu. Alikuwa na shauku na majaribu kama nasi pia tulivyo nayo. Bibilia ilisema alikuwa nayo. Alikuwa mwanadamu, si Malaika aliye juu ya majaribu.*

**Waebrania 1:4** *ilisema Yeye amefanyika bora kupita malaika. Alikuwa mwanadamu, mwanadamu kabisa, kwamba Mungu alichukua mwanadamu kamili kuleta ukombozi mkamilifu; na **Yeye akamjaza na Roho wake; Roho Mtakatifu alikuwa ndani yake bila kipimo.** Naye alijaribiwa kama tulivyojaribiwa. Naye alikuwa Mungu kabisa. Alithibitisha hilo alipofufua wafu, alipokomesha maumbile. Bahari iliponguruma na upepo mkali. Alipozungumzia miti, nakadhalika, vilimtii. Ndani alikuwa Mungu. Na angeweza kuwa mwanadamu **kwa kuwa alikua mwanadamu lakini yeye kwa ukamilfu wote akajipeana kabisa kama mwanadamu katika mikono ya Mungu** kwa ajili ya huduma ya Mungu. Na yeye ni mfano kwetu.*

**Utuonyeshe Baba, yatutosha:** **56-0422 E-36** *Sasa, ni mara nyingi imesemekana kwamba hakuna mwanadamu awezaye kumuona Mungu wakati wowote, Biblia ilisema hivyo. Bali Mwana wa peke wa Baba amemtangaza. Filipo, hapa alikuwa na maswali sana, alitaka kumuona Baba. Inasema hapa alisema “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Alisema “Aliyeniona mimi amemwona Baba;” kwa maneno mengine, unamuona **Baba akijieleza mwenyewe kupitia kwa Mwana.** **Yeye na Baba walikua mmoja jinsi ya kwamba Baba alikaa ndani yake.** Si yeye akifanya zile kazi; alikuwa Mwana, yeye mwenyewe, asiyekufa, aliyezaliwa na bikira, Mwana wa Mungu. Halafu yule Mungu alikaa ndani yake, Yule Baba, akijieleza mwenyewe kwa ulimwengu, sifa yake ikielekea watu, unaona? Vema, hivyo ndivyo Kristo na Mungu walivyokuwa mmoja. “**Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake.**” Sasa, alisema “**Unaponiona mimi amemwona Baba basi wewe wasemaje, ‘Utuonyeshe Baba?’**”*

**Sisi Tungemwona Yesu 58-0612 Kifungu55** *alipokuwa hapa ardhini, wangapi wanajua ya kwamba hiyo ilikuwa ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli jangwani, kwamba ilikuwa Kristo, yule Malaika wa agano? Vyema. Wangapi wanajua yule alikuwa **Yesu ndani ya Yesu, roho yule yule??***

**Kufunuliwa Kwa Mungu 64-0614 259** *Kama Yesu aliyowahi kusema, “Unaponiona Mimi, umemuona Baba”. Unaona? Mungu na Neno Lake ni Mmoja. Sasa mnaelewa? Wakati Neno linapodhihirishwa, ni nini? Unaona? 260 Yesu alisema, “Chunguzeni Maandiko, mnafikiri mnao... Mnamwamini Mungu, niaminini na Mimi pia. Kama sizitendi kazi za Baba yangu, basi msiniamini. Lakini kama nikitenda hizo kazi, Mimi na Baba Yangu tu Mmoja. Unaponiona Mimi umekwishamwona Baba. Na **unapoona Neno likifanywa dhahiri, unamuona Mungu Baba, Kwa sababu Neno ndiye yule Baba, Neno ndiye Mungu.** Na Neno likifanywa dhahiri ni Mungu mwenyewe akichukuwa neno lake na kulieleza mionganini mwa waaminio.*

**Kitendawili 61-1210 253** Yesu alitenda kazi za Babake **kwa sababu Baba alikuwa ndani yake.** Hiyo ndio ilikuwa sababu ya zile kazi kutendeka, **kwa sababu Baba alikuwa ndani ya Mwana.** Mnaamini hilo? Kwamba **ndani yake**, Yeye alikuwa Mungu aliyefanyika mtu. Mnaamini hilo? Kwamba **Mungu Baba, ambaye ni Baba wa Yesu Kristo, Yule Roho mkuu alikaa kwa utimilfu wa nguvu ndani ya Yesu Kristo, ambaye alikuwa hekalu la Mungu, aliyefanyika mwili wa nyama na kukaa ardhini, akiakilisha lile Neno.**

**Kitendawili 61-1210 315** Mimi ninaamini kwamba **Yesu ni Mwana wa Mungu aliye hai,** aliyezaliwa na bikira, alichukuliwa mimba, Mungu ndani ya tumbo la uzazi, **hekalu ambalo angekaa ndani yake.** Naamini hivyo, **ndani ya Kristo, Yeye ni Mungu aliyefanyika mtu.** Ni **Mungu aliyefanyika mwili wa nyama.** Baba Mungu alipokuja ndani ya Yesu kristo, Yeye alikuwa ule utimilifu wa Uungu **mwilini; ndani yake kulikaa utimilifu wote.** Mungu Baba aliyasema Maneno. Yesu alisema, “**Mimi sineni jambo lolote; lakini Baba akaaye ndani yangu. Yeye hunena.**”

Katika kufunga ningependa kuonyesha hoja nane za Ukweli Wa Mambo au matamshi yanayoeleza namna William Branham alivyotufundisha Uungu

**UKWELI WA MAMBO No.1)** Ndugu Branham “**Alikanusha kuwa alikuwa wa fundisho la Umoja**”

**Kwelezewa kwa Uungu E-74** Wengi wa nyinyi watu mnaosikia haya mngesema, “Ndugu Branham ni wa Umoja” Sivyo. Nafikiri nyinyi wote mumekosea, wa umoja na wa utatu pia, si kutofautiana tu, mara zote inapaswa kuwa katikati mwa njia.”

**UKWELI WA MAMBO No.2)** Ndugu Branham alisema “**Mungu na Yesu si mmoja kama kidole chako kilivyo.**

E-96 **Utuonyeshe Baba** 53-0907.1A Kuna Mungu mmoja tu. Na ninatofautiana na sikubaliani na muungano wa wapentekote unaoita ule umoja kama kidole chako kimoja kilivyo. Hilo ni kosa. Bila shaka, ni kosa.

**UKWELI WA MAMBO No.3)** Ndugu Branham alisema “**Yesu asingeweza kuwa baba wa Yeye mwenyewe.**”

128 **WAEBRANIA SURA YA NNE** 141-126 - 57-0901 2E Sasa wale wa dehebu la Oneness walilichukua hilo, lile kundi la watu wa Oneness, na kujaribu kufanya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, afisi moja tu na mahali pamoja, na kama kidole chako, kimoja. Hilo ni kosa. Mungu hangeweza ... Yesu hangeweza kuwa Baba Yake Mwenyewe. Ikiwa alikuwa Baba Yake Mwenyewe, basi yeye alikuwa ... Vema, jinsi gani Yeye angeweza kuwa Baba yake Mwenyewe?

**UKWELI WA MAMBO No.4)** Ndugu Branham alisema “**kuna utofauti kati ya Baba na Mwanawe**”

**WAEBRANIA SURA YA SABA** Sehemu 1 57-0901 2E *Sasa, sababu kukawa na tofauti kati ya Mungu na Yesu: Yesu alikuwa na mwanzo, Mungu hakuwa na mwanzo; Melkizedeki hakuwa na mwanzo, na Yesu alikuwa na mwanzo.* Lakini Yesu alifananishwa na Yeye.

**UKWELI WA MAMBO No.5)** Ndugu Branham alisema “*Mungu hakuwa ndani ya Yesu hadi alipobatizwa mtoni Yordani.*” Na “*Mungu alimuacha katika Gethsemane apate kufa kama wote wanaokufa.*”

**282 Kitendawili 64 0206.1M** *Na maskini Mvulana huyu, Mtoto mwenye umri wa miaka kumi na miwili, hana elimu hata kidogo, mbona, bali ni Mvulana tu mwenye umri wa miaka kumi na miwili. Baba hakuwa akiishi ndani Yake wakati huo; kwa maana alikuja kwenye siku aliyombatiza, “Alimwona Roho wa Mungu akishuka, unaona, na akaingia ndani Yake.” Lakini, angalia, maskini Mvulana huyu mwenye umri wa miaka kumi na miwili, akiwa Neno; Yeye alizaliwa Aliyetiwa Mafuta, unaona, apate kutiwa mafuta. Naye ndiye huyu hapa, “Hamjui ya kwamba inanibidi kufanya kazi ya Baba yangu?”*

Tazama Ndugu Branham anatwambia ya kwambaalikuwa bado hajakaa ndani ya Yesualipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili. Anatwambia ya kwamba Mungu aliingia ndani ya mwanawe Mtoni Yordani alipobatizwa na Roho Mtakatifu.

**Yule Nabii Eliyah** 56-1002 2E E-21 “*Na Yesu, ule ubatizo aliyokuwa nao ulikuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao ulikuwa ndani yake, uliokuja juu yake pale mtoni Yordani baada ya kubatizwa kwa maji.* Yohana alishuhudia kwamba; aliona Yule Roho wa Mungu mfano wa njiwa akimjia. Na tazama. Halafu alipopanda juu, alirudisha vazi lile lile alilovishwa: yaani Roho Mtakatifu juu ya Kanisa.

**Wana wa Mungu Walioadhimishwa:** 60-0518 88 “*Katika Bustani ya Gethsemane, ule upako ulimuondoka, unajua, Ilimpasa yeye kufa akiwa mwenye dhambi. Alikufa akiwa mwenye dhambi, unajua hivyo; si dhambi zake, bali zangu na zako.*

**Ni kule kuchomoza kwa jua** 65-0418 “*Wakati Mungu alipoangalia chini katika ule mwili 241 (Roho alimwacha Yeye, kwenye Bustani ya Gethsemane).* Alipaswa kufa, akiwa mwanadamu. Kumbukeni, marafiki, haikumpasa kufanya jambo hilo. Huyo alikuwa Mungu. Mungu aliutia ule mwili mafuta, ambao ulikuwa mwili wa binadamu. Na haikumbidi... Kama angalienda pale juu kama Mungu, Yeye asingalikufa kifo cha namna ile kamwe; huwezi kumwua Mungu.

**Kutamalaki Malango ya Adui** 59-1108 **Kifungu 47...***Roho Mtakatifu alipomjia katika ubatizo wa Yohana, na akafanyika Yule Masihi mpakwa mafuta... Sasa kumbuka, Yeye alikuwa Mwana wa Mungu alipozaliwa. Alikuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira.* Lakini alipofanyika Masihi, hapo ndipo Roho Mtakatifu alipomjia, kwa sababu Yule “masihi” maanake ni “mpakwa mafuta.” Unaona? Naye alikuwa aliyepakwa mafuta Roho mtakatifu alipomjia...

**E- 40 Ushuhuda wa William Branham** 60-0210 *Mungu Yule aliyekutana na Musa jangwani, alikuwa ndani ya Yesu Kristo ardhini, kwa kuwa maisha yake yanashuhudia kwamba ni Roho Yule Yule. Inatenda jambo lile lile.*

**UKWELI WA MAMBO No.6) Ndugu Branham alisema “Mwili wa Yesu haukuwa Uungu, bali Uungu (Mungu) ulikaa katika ule Mwili”**

**Kristo aliyetambulishwa katika vizazi vyote 64-0617 36 Sasa, tazama sasa, Mungu... Yesu alisema wale waliojiliwa na neno la Mungu waaliitwa miungu; hao walikuwa manabii. Sasa, si mwanadamu mwenyewe aliyekuwa Mungu, zaidi ya vile mwili wa Yesu Kristo usingeweza kuwa Mungu. Yeye alikuwa Mwanadamu, na Mungu alifunikwa nyuma yake.**

**Karama za Mungu kila mara hupata panapofaa 63-1222 93 yule mwanadamu, mwili haukuwa uungu, uungu ulikuwa ndani ya ule mwili.**

**E-37 Msingi wa kanuni za imani 55-0113** Sasa, alipokuwa hapa ardhini, yeye alikuwa mfano kamili wa kila kipengele cha uungu. Alikuwa utimilifu wa ule Uungu mwilini. **Mungu alikaa ndani ya Kristo. Mwili wa Kristo ulikuwa tu hekalu la Mungu. Hapo ndipo Mungu mwenyezi aliishi na kukaa ndani ya mwili wa kiumbe cha kibinadamu. Mnaamini hilo, sivyo? inakupasa kuamini, ili uokoke.** Inakupasa kuamini hivyo.

**UKWELI WA MAMBO No. 7)** Ndugu Branham anatuambia “Mungu alipomzaa Yesu kulikuweko viumbe viwili vilivyo husika” Mmoja ambaye ni Mungu na mmoja ambaye ni Mwana wa Mungu.

**Hali ya hisia na Mungu ni nani? 50-0815 018** Lakini aliyaandika katika mbingu, ya kuwa mwanadamu angeangalia juu na kutambua ya kwamba Yule muumbaji Jehova aliishi juu. Na sasa naweza kumuona, aliangalia pale...ninaweza kumuona akinena na dwara hii ikininginia pale kama kishungi cha barafu, chochote kile ilichokuwa, kule mbali. Na akaisongesha hapa hivi. Naweza kuona nuru hiyo ndogo ikitokezea. Sasa, **TUKO NA WAWILI.** Baba, na kutoka kwa Baba ikaja Nuru, Yule Mwana. Na ninaweza kuona ile nuru ikisonga hapa juu na ikavuta ardhi juu karibu na jua kuikausha. Na kuanza ku...? Kuinua maji juu, ikiyatetenganisha na nchi, Ardhi ikitengana na yale maji, nakadhalika.

Si Miungu wawili. Kuna Mungu mmoja naye alikuwa na Mwana. Maandiko yanamuita “Mwana wa Mungu”, kamwe hayajasema kwamba yeye ni “Mungu mwana”.

**Maswali juu ya Kitabu cha Mwanzo 53-0729 007 Katika Mwanzo 1:26** hebu na tupate ile sehemu ya kwanzia kwanza. Mungu alisema “hebu sisi tu...” Sasa, (sisi) ni... ”Na tumfanye mtu kwa mfano wetu.” Wetu, bila shaka, tunatambua anasungumza na mtu fulani; **Yeye alikuwa akisema na kiumbe kingine.** Na (sisi) tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale wanyama walio juu nchi.”

**Pasia ya Wakati 55-0302 E-22** hawangeweza kumwelewa. Yeye alikuwa fumbo, hata kwa wale Mitume. Hakuna aliymwelewa, kwa sababu **kulikuwa na watu wawili wakinena wakati wote.** - 23 **Mtu Yesu Kristo alikuwa akinena, na Mungu alikuwa akinena ndani yake, pia. Wakati mwingine ilikuwa ni Kristo mwenyewe, wakati mwingine ilikuwa Yule baba aliyekaa ndani yake.** Unaiona? Yeye - hawangeweza kuelewa mambo fulani yeye angesema; Yeye alinena nao kwa mafumbo.

**UKWELI WA MAMBO No.8)** Ndugu Branham alisema “**Yesu alikuwa na maumbile ya viumbe viwili, kwa sababu Mungu aliishi ndani yake.**”

**Utuonyeshe Baba, yatutosha:** 56-0422 E-36 Filipo, hapa alikuwa na maswali sana, alitaka kumuona Baba. Inasema hapa alisema “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Alisema “Aliyeniona mimi amemwona Baba;” **kwa maneno mengine, unamuona Baba akijieleza mwenyewe kupitia kwa Mwana.** Yeye na Baba walikua mmoja kwa shauri ya kwamba Baba alikaa ndani yake. Si yeye akifanya zile kazi; alikuwa Mwana, yeye mwenyewe, asiyekufa, aliyezaliwa na bikira, Mwana wa Mungu. Halafu ndani yake alikaa Mungu, Yule Baba, akijieleza mwenyewe kwa ulimwengu, sifa yake ikielekea watu, unaona? Vema, hivyo ndivyo Kristo na Mungu walikuwa mmoja. “**Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake.**” Sasa, alisema “Unaponiona mimi amemwona Baba basi wewe wasemaje, ‘Utuonyeshe Baba?’”

**KARAMA 56-1207 E – 29** Sasa, **ndani ya Kristo** kulikaa ule utimilifu wa Uungu mwilini, yeye alikuwa na Roho wote wa Mungu ndani yake. Mimi na Baba yangu tu umoja alisema Yesu. Hiyo ndio sababu watu wasingemwelewa. **Wakati mwingine angesema jambo fulani, ingeonekana kana kwamba aliligeuza na kusema jambo tofauti. Ilikuwa ni yeye akinena, kisha Baba akanena.** Unaona? Wao walikuwa... na hata wale wanafunzi wasingemwelewa. Na mwishowe kabisa walisema “Tazama, sasa wasema waziwazi. Sasa tumejua ya kuwa wewe wafahamu mambo yote, wala huna haja ya mtu akuulize” Yesu akawajibu, Je! Mnasadiki sasa? Baada ya muda huo wote, wasingelipata ile...mbona? Kwa kuwa wakati mwingine alisema hivi kisha akasema vile. **Ilikuwa yeye na Baba wakinena.** E-30 Tazama kwa makini. Sasa **Mungu akikaa ndani ya Kristo alitumia sauti yake kunena nayo.** Yesu alisema kuhusu muujiza wake, “Amin, amin, nakuambia, Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.” Hiyo ni sawa? Mtakatifu Yohana 5:19 **Kwa hivyo hakutenda jambo lolote kwa uwezo wake mwenyewe. Hakuna nabii aliyetenda lolote kwa uwezo wake mwenyewe, hadi Mungu alipoonyesha la kutenda.** Ni kosa kuu jinsi gani alilofanya Musa alipoondoka bila ono la Mungu na akampiga chini na kuua yule Mmisri. Alidhani angewaweka huru kwa mikono yake, kwa vile alifikiri alikuwa na imani nydingi, kwa sababu alikuwa ameitwa kwa ajili ya ile kazi. **Haijalishi kwa jinsi gani umeitiwa hiyo kazi, ni lazima Mungu atende kazi ya kuelekeza.** Unaona? Alishindwa kwa elimu yake yote na akili zake za kivita na mafundisho aliopata kama kiongozi mkuu wa Kimisri. Hata hivyo ilishindwa, kwa sababu **Mungu alikuwa na mpangilio na inatupasa kutenda kazi kulingana na mpangilio wa Mungu.** Haijalishi ni nini tunachofanya, jinsi gani tulivyo hodari, imetupasa kunyeyekeea na Kutenda kazi kulingana na mpangilio wa Mungu. Amina. Kwa hivyo alishindwa na ilimbidi Mungu kumweka miaka arobaine mingine kumwelimita. Basi ilivyokuwa, ilimlazimu yeye kujisahau mwenyewe, hadi hakuwa yeye, bali ilikuwa ni Mungu.

**Aliapa kwa Yeye mwenyewe 53-1212** Yeye alisema, Mimi na Baba yang tu Mmoja. “Baba yangu yu ndani yangu” akasema “utuonyeshe Baba” Filipo alisema. “Unionyeshe mimi Baba na itanitosha” akasema, “Filipo, nimekuwapo pamoja nanyi kwa muda mrefu, wewe usinijue mimi? Yeye akasema, “unaponiona mimi, unaona Baba.” Basi wasemaje, ‘nionyeshe Baba.’ Mimi na Baba tu mmoja. **Baba yangu anaishi ndani yangu.** Si mimi nitendaye hizo kazi, ni yeye akaaye **ndani** yangu, anayetenda hizo kazi.” Oh, mie. Ningewezaje kumwambia mtu kilicho kasoro naye? Ningewezaje kumweleza yatakayomtokea miaka kumi ijayo, au alichokuwa miaka arobaine iliopita? Si mimi. Halleluyah. **Ni yeye aishiye ndani yangu,** aliyeshuka chini, kwamba kupidia damu yake alinileta katika ushirika naye. Halleluyah. Mikono yangu ingewezaje kufanya lolote kwa kuponya wagonjwa? Haina nguvu hata kidogo. Si mimi. **Bali ni yeye anayekaa hapa ndani anayelitenda.**